*Mulika, Na. 43 (2), 197-210*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uchanganuzi wa Kirai Kihusishi cha Kiswahili

*Tumaini Mahendeka*[1]
Taasisi ya Elimu Tanzania
na
*Luinasia E. Kombe*[2]
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na43t2.1

**Ikisiri**

Makala haya yanajadili muundo wa kirai kihusishi cha Kiswahili kwa kutumia mkabala wa sarufi miundo virai. Yanatambua kategoria tano za virai katika Kiswahili: virai nomino, virai kitenzi, virai kivumishi, virai kielezi, na virai kihusishi. Wataalamu wa sarufi ya Kiswahili wamekuwa wakitumia mkabala huu kuelezea muundo wa kirai kihusishi, lakini wanatofautiana kuhusu vijenzi vinavyohusishwa, jambo linalosababisha ukosefu wa urari katika uchanganuzi. Lengo la makala haya ni kubainisha muundo wa kirai kihusishi cha Kiswahili, kueleza sifa zake za kimuundo, na kufafanua sababu za kiisimu zinazowafanya wataalamu kutofautiana kuhusu uchanganuzi wa vijenzi vya kirai kihusishi licha ya kutumia mkabala mmoja wa sarufi miundo virai. Data zilichambuliwa kwa mbinu ya uchambuzi wa matini na mbinu ya uchambuzi wa maudhui. Matokeo yanaonesha kuwa kirai kihusishi kinaundwa na kihusishi kama neno kuu na kirai nomino au kishazi tegemezi kama vijalizo vyake. Neno kuu la kirai hutawala vijalizo vyake na halisimami peke yake. Aidha, matokeo yanaonesha kuwa tofauti za kiisimu zinazofanya wataalamu watofautiane kuhusu uchanganuzi wa vijenzi za kirai kihusishi zinatokana na athari za tafsiri kutoka Kiingereza na kutokuzingatia kanuni za miundo virai.

## 1.0 Utangulizi

Dhana ya kirai imefasiliwa na baadhi ya wataalamu. Miongoni mwa wataalamu hao ni TUKI (2019) ambayo inaeleza kwamba kirai ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi. Kirai ni tungo yenye neno moja au zaidi ambayo uhusiano wake umekitwa katika neno kuu ambalo ndio msingi wa mwandamano wa maneno mengine katika kirai. Katika uchanganuzi wa kawaida, kirai huweza kuwa neno kuu peke yake au neno kuu na neno/maneno yanayoteuliwa yanayoteuliwa kuandamana nalo. Kwa kawaida, katika lugha ya Kiswahili,

[1] **Baruapepe:** tumaini.mastjabu@tie.go.tz
[2] **Baruapepe:** luinasia.kombe@duce.ac.tz

neno kuu hukaa mwanzoni katika mwandamano (Khamis, 2009; Kihore, 2009). Kwa kutumia dhima za kisarufi, Kimani, Mwihaki na Buliba (2006) wanafasili kirai kuwa ni fungu la maneno lisilokuwa na kiima wala kiarifu chake. Pia, Trask na Stockwell (2007) wanaeleza kwamba katika isimu mamboleo, istilahi kirai hutumika kuonesha kiambajengo chochote cha kisintaksia katika sentensi.

Vilevile, wataalamu mbalimbali wa Kiswahili wanafafanua kuwa kirai kihusishi (kunzia sasa KH) ni kipashio cha kisintaksia ambacho hutawaliwa na kihusishi kama neno kuu (OUT, 2018; Wesana-Chomi, 2017). Kirai kihusishi kina tabia tofauti na virai vingine kwa kuwa neno kuu haliwezi kusimama peke yake. Kwa mujibu wa Downing (2015), katika virai vingine neno kuu linaweza kusimama peke yake bila kijalizo[3] na kufanya kazi kama kirai chenyewe ilhali neno kuu la kirai kihusishi haliwezi kusimama peke yake bila kijalizo chake. Hivyo, bila kijalizo hakuna kirai kihusishi. Kwa mfano, *katika shida*, *mpaka asubuhi*, *cha mchana*, *wa nidhamu* ni virai vihusishi. Maneno makuu katika virai vihusishi hivyo ni *katika*, *mpaka*, *cha* na *wa* mtawalia. Muundo wa kirai kihusishi ni kihusishi na kijalizo chake ambacho ni KN [shida, asubuhi, mchana, nidhamu]. Katika mifano hiyo, neno kuu haliwezi kusimama lenyewe kwa sababu halina ujazo wa kisemantiki. Hivyo, makala haya yanakubaliana na hoja ya Downing kwamba neno kuu la kirai kihusishi haliwezi kusimama peke yake bila kijalizo chake kwa kuwa halina ujazo wa kisemantiki.

Kumekuwapo na makundi mawili ya wataalamu wa sarufi ya Kiswahili ambayo yamekuwa yakieleza muundo wa KH cha Kiswahili kwa namna tofauti ilhali yanatumia mkabala mmoja, yaani sarufi miundo virai (kuanzia sasa SMV). Kwa kuwa makundi yote yanatumia mkabala mmoja, tulitegemea kuwe na urari katika uchanganuzi wa muundo wa kirai kihusishi lakini jambo hili halijitokezi.


Kundi la kwanza la wataalamu ni lile linaloona kwamba KH kinaundwa na kihusishi ambacho ni maneno mawili na kijalizo chake ambacho ni kirai nomino. Wataalamu hawa wanaeleza kwamba vifungu vya maneno kama vile *mbele ya meza*, *chini ya mti*, *nyuma ya nyumba*, *ndani ya shimo*, *juu ya kabati* na *kando ya barabara* ni virai vihusishi. Wanaendelea kueleza kwamba vimeundwa na vihusishi ambavyo ni *mbele ya*, *chini ya*, *nyuma ya*, *kando ya*, *ndani ya* na *juu ya* pamoja na vijalizo ambavyo ni virai nomino. Kwa mtazamo wa watalaamu hawa, neno kuu limeundwa na maneno mawili, yaani neno huru zaidi ya moja. Miongoni mwa wataalamu wa mtazamo huo ni Kapinga (1983), Habwe na Karanja (2004), Matei (2008) na Matinde (2012).

Kundi la pili la wataalamu ni lile linaloona kwamba KH kinaundwa na kihusishi ambacho ni neno moja na kijalizo chake ambacho ni kirai nomino. Wataalamu

[3] Kijalizo ni kipashio cha lazima kinachokamilisha neno kuu ambapo kinaweza kuwa neno moja au kifungu cha maneno (mawili au zaidi)

hawa wanaeleza kwamba vifungu vya maneno kama *ndani ya shimo*, *nyuma ya nyumba*, *mbele ya meza*, *chini ya mti*, *juu ya kabati na kando ya barabara* sio virai vihusishi. Kwao, virai vihusishi ni sehemu ya vifungu hivyo ambayo ni *ya shimo*, *ya nyumba*, *ya meza*, *ya kabati* na *ya barabara*. Katika uchanganuzi wao, wanaeleza kwamba virai hivyo vimeundwa na kihusishi ambacho ni neno moja [*ya*] na virai nomino *shimo*, *nyumba*, *meza*, *mti*, *kabati* na *barabara*. Virai vihusishi [ya shimo, ya nyumba, ya meza, ya mti, ya kabati, ya barabara] vinakumusha nomino za mwanzo ambazo ni *ndani*, *nyuma*, *mbele*, *chini*, *juu* na *kando.* Miongoni mwa wataalamu wa sarufi ya Kiswahili wenye mtazamo huu ni Mychina (1981), Amidu (2004) na Wesana-Chomi (2017).


Kundi la kwanza linachanganua virai vihusishi kama Kielelezo Na. 1 (a) na (b) kinavyoonesha.




**Kielelezo Na. 1: Uchanganuzi wa KH chenye H cha Maneno Mawili na KN**
**Chanzo:** Kapinga (1983), Rubanza (2003) na Habwe na Karanja (2004)


Kielelezo Na. 1 (a) kinaonesha kuwa KH ni [juu ya meza] ambacho kimeundwa na kihusishi [juu ya] na nomino [meza] ilhali Kielelezo Na. 1 (b) kinaonesha kuwa KH ni [nyuma ya nyumba] ambacho kimeundwa na kihusishi [nyuma ya] na nomino [nyumba].

Amidu (2004) anatoa maelezo tofauti ukilinganisha na watangulizi wake. Anadai kwamba uchanganuzi katika Kielelezo Na.1 (a) na (b) si sahihi kwani tungo kama vile *juu ya meza* na *nyuma ya nyumba* si virai vihusishi bali ni virai nomino ambavyo ndani yake kuna virai vihusishi. Hivyo, KH ni *ya meza* na *ya nyumba* ambapo neno kuu ni kihusishi *ya* na kijalizo chake ni nomino [meza, nyumba]. Kwa hiyo, virai vihusishi *ya meza* na *ya nyumba* vimeundwa na kihusishi [ya] kama neno kuu na vijalizo vyake ambavyo ni nomino, yaani *meza* na *nyumba*. Kutokana na ufafanuzi wa Amidu (2004), ni wazi kuwa virai vihusishi [ya meza, ya nyumba] vinakumusha nomino *juu* na *nyuma* kama Kielelezo Na. 2(a) na (b) kinavyodhihirisha.




**Kielelezo Na. 2: Uchanganuzi wa KH chenye H cha Neno Moja na KN**
**Chanzo:** Amidu (2004: 48)

Aidha, Wesana-Chomi (2017) anaongezea kwa kueleza kwamba kuna virai vihusishi ambavyo hutokea vikiwa vinakumusha KN changamani na hufanya kazi kama vivumishi. Kielelezo Na. 4 (a) na (b) kinaonesha virai vihusishi vinavyokumusha virai nomino katika muundo wa viambajengo.




**Kielelezo Na. 3: Uchanganuzi wa KH Kinachokumusha KN**
**Chanzo:** Wesana-Chomi (2017: 120)

Kwa mujibu wa Wesana-Chomi (2017), Kielelezo Na. 3 (a) na (b) kinaonesha kuwa vifungu vya maneno *ya dhahabu* na *wa kushoto* ni virai vihusishi ambavyo vinakumusha nomino [pete, upande].

Uchanganuzi wote wa wataalamu wa kundi la kwanza na la pili kuhusu KH cha Kiswahili unatofautiana. Hivyo, makala haya yanalenga kubainisha muundo sahihi wa KH kwa kueleza sifa za kimuundo za kirai kihusishi na kufafanua sababu za kiisimu zilizowafanya wataalamu wa sarufi ya Kiswahili kutofautiana kiuchanganuzi, jambo ambalo litasaidia kuongeza maarifa, hususani katika eneo la uchanganuzi wa KH.

## 2.0 Nadharia ya Utafiti

Uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Sarufi Miundo Virai (kuanzia sasa NSMV) iliyoasisiwa na Noam Chomsky miaka ya 1950. NSMV ilitumika kwa sababu ni nadharia inayohusu uchanganuzi wa viambajengo vya virai. Obuchi na Mukhwana (2015) wanaeleza kwamba uchanganuzi wa kisintaksia haukamiliki pasi na kurejelea sarufi miundo virai na kanuni zake ambazo ni neno kuu, kategoria ya kileksika, umiliki na usabiki wa vifundo dada. Kanuni hizi zina uwezo wa kuzalisha ruwaza za elementi za kiisimu. Nadharia ya Sarufi Miundo Virai ina misingi mikuu mitatu. Msingi wa kwanza ni kwamba kila lugha ina upekee wake na sentensi ya lugha inawakilishwa na seti ya viambajengo na si kiambajengo kimoja kama ilivyo kwenye ngazi ya fonimu, mofimu au maneno. Msingi wa pili ni kwamba katika mfumo wa muundo kirai, kila kiambajengo kinawakilisha dhana fulani. Hivyo, kirai kina viwakilishi vingi tofauti. Kwa mfano, tungo *Mtu alipiga mpira* ni sentensi inayowakilishwa na viambajengo KN na KT. Kiambajengo KN kinawakilishwa na *Mtu* na kiambajengo KT kinawakilishwa na *alipiga mpira*. Msingi wa tatu ni kwamba, uchanganuzi wa sentensi na virai sharti ufanywe kwa kuvigawa katika sehemu mbalimbali ili kufafanua vijenzi vya tungo. Nadharia ya Sarufi Miundo Virai imejikita katika mhimili wa ngazi leksika. Mhimili huu unahitaji viambajengo katika kirai kupangwa katika mpangilio wa kingazi msonge ambapo viambajengo hupangwa hatua kwa hatua ili kujenga viambajengo vikubwa zaidi vinavyokubalika kwa wazungumzaji wazawa wa lugha husika. Chomsky (1957) anaeleza kwamba mhimili wa ngazi leksika ni mchoroti wenye maelezo kuhusu muundo wa viambajengo vya sentensi vinavyojengwa na kanuni zinazozalisha sentensi na huwa na taarifa chache kutoka katika kanuni miundo virai.

## 3.0 Mbinu za Utafiti

Data zilizotumika katika makala haya zimepatikana katika machapisho yanayohusu sarufi ya Kiswahili. Machapisho hayo ni vitabu na makala. Katika kufikia malengo ya makala haya, mtafiti alitumia mbinu ya uchambuzi wa matini ambapo alisoma na kuchambua matini za sarufi ya Kiswahili, hususani vitabu na makala kuhusu uchanganuzi wa KH cha Kiswahili kama vyanzo vya data kwa kuwa mbinu hiyo ilikuwa inaendana na lengo la makala haya. Katika kupata data toshelevu, mtafiti alisoma sampuli ya matini saba za sarufi ya Kiswahili. Data zilichambuliwa kwa mkabala wa kitaamuli, kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui. Kadhalika, mchoroti ulitumika kuweka wazi uchanganuzi wa KH cha Kiswahili. Lengo lilikuwa kuonesha mpangilio wa viambajengo katika udarajia na uhusiano wa viambajengo kiumiliki.

## 4.0 Muundo wa KH cha Kiswahili

Makala haya yamebaini kwamba, muundo wa KH cha Kiswahili umejikita katika kihusishi (H) na kirai nomino (KN) pamoja na kihusishi na kishazi tegemezi/rejeshi (Kg).

### 4.1 Muundo wa Kihusishi (H) na Kirai Nomino (KN)

Kimuundo, KH cha Kiswahili kinaundwa na neno kuu ambalo ni kihusishi (H) na kijalizo chake ambacho ni KN. Kwa upande wa neno kuu, kipashio lazima kiwe cha kategoria ya kileksika na liwe neno moja. O'Grady (1996) anaeleza kwamba kategoria ni kiwango cha neno mojamoja la kileksika ambalo linaweza kuwa nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi au kihusishi. Kwa upande wa kijalizo, vipashio vinaweza kuwa vya kileksika au kirai kama ilivyo katika Data Na.1 na 2.

1. (a) ya nyumba
   (b) katika nyumba
   **Chanzo:** Amidu (2004: 50)

2. (a) kwa fedha taslimu
   (b) kwa shemeji yake
   (c) Mtu aliye kando haangukiwi na mti wowote.
   **Chanzo:** Kapinga (1983: 186-187)


Tungo zilizopigiwa mstari katika Data Na. 1 na 2 ni virai vihusishi vilivyoundwa kwa maneno makuu ambayo ni vihusishi [ya, katika, kwa, na] na vijalizo vyake ambavyo ni virai nomino [nyumba, fedha taslimu, shemeji yake, mti wowote].

### 4.1.2 Kihusishi (H) na Kishazi Tegemezi/Rejeshi

Pia, KH kinaweza kuundwa na kihusishi kama neno kuu na kishazi rejeshi au tegemezi kama kijalizo chake. Kishazi tegemezi ni kishazi ambacho hakiwezi kujikamilisha kimaana bali hutegemea kishazi huru. KH huweza kuundwa na kihusishi na kishazi tegemezi kama inavyoonekana katika Data Na. 3.

3. (a) Neno la Bwana linasema ya kwamba Hagai alimzaa Yonamu.
   (b) Amepewa kipigo kwa alichokifanya usiku wa kuamkia leo.
   **Chanzo:** OUT (2018: 123-124)

Data Na. 3 (a) na (b) zinaonesha kuwa vifungu vya maneno vilivyopigiwa mistari ni virai vihusishi ambavyo vimeundwa na vihusishi [ya, kwa] pamoja na vishazi tegemezi ambavyo ni vijalizo vya vihusishi hivyo. Hivyo, KH huweza kuundwa na kihusishi na kishazi tegemezi kama Kielelezo Na. 5 kinavyoonesha.




**Kielelezo Na. 4: KH Kilichoundwa kwa H na Kg**
**Chanzo:** OUT (2018: 124)

Kielelezo Na. 4 kinadhihirisha kwamba KH kinaundwa na kihusishi [kwa] na kishazi tegemezi [alichokifanya usiku wa kuamkia leo]. Kimuundo, KH huweza kuundwa na kihusishi kama neno kuu na kishazi tegemezi kama kijalizo chake. Ni dhahiri kuwa KH hakiundwi na kihusishi na KN pekee, bali kinaweza kuundwa na kihusishi na kishazi tegemezi. Hivyo, kishazi tegemezi ni mojawapo ya vijalizo vya kihusishi.

### 4.2 Sifa za Kimuundo za Kirai Kihusishi cha Kiswahili

Makala haya yamebaini kwamba KH cha Kiswahili kina sifa za kimuundo zipatazo tano ambazo ni: neno kuu la kirai kuwa kihusishi; neno kuu kutawala vijalizo vyake; neno kuu kutangulia kijalizo chake; neno kuu kutosimama peke yake, na KH kuundwa na viambajengo au vipashio vya kileksika upande wa neno kuu na/au vipashio vya kileksika, kirai au kishazi tegemezi kwa upande wa kijalizo.

#### 4.2.1 Neno Kuu la Kirai kuwa Kihusishi

Makala haya yamebaini kwamba, kimuundo KH cha Kiswahili kina sifa ya kuundwa na neno kuu. Kihusishi ndicho neno kuu ambalo ni la lazima na muhimu kisemantiki. Viambajengo vinavyoambatana na neno kuu vimejengwa juu yake kama inavyoonekana katika Data Na. 4.

4. (a) kabla ya saa tatu asubuhi
(b) ya nyumba
(c) ya mti
(d) kwa msaada
**Chanzo:** Matei (2008: 78)

Data Na. 4 (a)-(d) inaonesha virai vihusishi. Katika virai vihusishi hivyo, neno kuu ni *ya* na *kwa* mtawalia. Data Na. 4 (a) inaonesha KH ambacho ni kiambajengo


ndani ya kirai kielezi (KE). KH [ya saa tatu asubuhi] ni kiambajengo kinachojenga KE [kabla]. Neno kuu la KH ambalo ni kihusishi [ya] ni la lazima na muhimu kisemantiki kwani likiondolewa sifa ya KH inapotea. Hivyo, kihusishi ni neno muhimu sana katika muundo wa KH. Tallerman (2015) na Hassan (2021) wanaeleza kwamba neno kuu la KH hubeba taarifa muhimu za kisemantiki na hubainisha maana ya kirai chote na haliwezi kudondoshwa au kuondolewa kwa kuwa ni la lazima. Aidha, sifa hii hujitokeza katika aina zote za virai.

**4.2.2 Neno Kuu Kutawala Vijalizo vyake**

Makala haya yamebaini kwamba, kimuundo, KH cha Kiswahili kina sifa ya neno kuu kutawala vijalizo vyake vinavyoambatana au vinavyoandamana nalo. Kutawala ni dhana inayohusu neno kuu la kirai kuamua neno la kuambatana nalo na kubainisha aina ya kirai ambapo sifa hii hujitokeza katika aina zote za virai. Hii inajidhihirisha katika Data Na. 5.

5. (a) wa shule
   (b) vyenye makali
   (c) wa Tanga
   **Chanzo**: Wesana-Chomi (2017:110)

Data Na. 5 inadhihirisha wazi kwamba neno kuu ambalo limepigiwa mstari linatawala vijalizo vyake ambavyo ni virai nomino [shule, makali, Tanga]. Kutokana na maneno makuu kutawala vijalizo vyake, yanaamua vijalizo vya kuandamana nayo na yanabainisha aina ya kirai kinachohusika kama inavyoonekana wazi katika Kielelezo Na. 5.





**Kielelezo Na. 5: Kihusishi Kinatawala Kirai Nomino**
**Chanzo:** Wesana-Chomi (2017: 10)

Kielelezo Na. 5 kinaonesha wazi kwamba kiambajengo H [wa] kinatawala kiambajengo KN [shule] kwa kuwa ndicho kinachobainisha aina ya kirai. Hii ni kwa sababu kiambajengo KN ni kitegemezi cha neno kuu. Hivyo, katika muundo wa viambajengo vya KH, kihusishi kinatawala KN ambacho ni kijalizo chake kama Baker (1995) na Miller (2002) wanavyoeleza kwamba neno kuu ni neno moja

ambalo linatawala kirai chote kwa kuwa ndilo linabainisha aina ya kirai na huamua kijalizo cha kuambatana nalo.

**4.2.3 Neno Kuu Kutangulia Kijalizo chake**

Makala haya yamebaini kwamba, kimuundo, KH cha Kiswahili kina sifa ya neno kuu kutangulia kijalizo chake. Utangulizani ni dhana ya uhusiano wa vifundo ambavyo vinafuatana kimstari au kiulalo kutoka kushoto kwenda kulia. Katika kubaini sifa hii, mtafiti aliongozwa na mhimili wa ngazi leksika wa NSMV. Mhimili huu ulimwezesha kubaini viambajengo vya KH vinavyotangulia viambajengo vingine kimstari kutoka kushoto kwenda kulia. Katika muundo wa KH cha Kiswahili, sifa hii hujitokeza pale ambapo kifundo dada kilichoko kushoto kinapokitangulia kifundo dada kilichoko kulia kama Kielelezo Na. 6 kinavyoonesha.




**Kielelezo Na. 6: Kihusishi Kimekitangulia Kijalizo chake**
**Chanzo:** Wesana-Chomi (2017)

Kielelezo Na. 6 kinaonesha uchanganuzi wa KH ambapo kihusishi [ya] kimeitangulia nomino [dhahabu] ambayo ni kijalizo chake. Neno kuu [ya] limetangulia kijalizo chake kwa sababu ni kifundo dada kilichoko kushoto mwa KN na kina nguvu katika mfuatano wa kiulalo au kimstari wa vifundo dada kutoka kushoto kwenda kulia.

**4.2.4 Neno Kuu Kutosimama Peke yake**

Kutokana na uchambuzi wa data, makala haya yamebaini kwamba, kimuundo, KH kina sifa ya neno kuu kutosimama peke yake. Neno kuu ambalo ni kihusishi halina uwezo wa kusimama peke yake, bali linahitaji kijalizo chake ambacho ni KN au kishazi tegemezi ili kujikamilisha kimaana. Data Na. 6 na 7 zinaonesha sifa hii.

6. (a) wa chifu huyo
   (b) kwa ugumu
   (c) wa kupigiwa mfano
   **Chanzo:** Matei (2008: 205)
7. (a) ya wizi
   (b) kwa sababu
   (c) wa somo

(d) hadi asubuhi
**Chanzo:** Obuchi na Mukhwana (2015: 77-78)

Data Na. 6 na 7 zinaonesha maneno yaliyopigiwa mistari ambayo ni vihusishi. Maneno hayo hayawezi kusimama peke yake bali yanahitaji vijalizo vyake ili kujikamilisha kimaana. Kwa mfano, vihusishi *wa, *kwa, *ya, na *hadi ni maneno ambayo hayawezi kusimama peke yake bila vijalizo vyake kwa sababu hayajikamilishi kimaana. Hivyo, sifa mojawapo ya kimuundo ya KH cha Kiswahili ni kwamba neno kuu haliwezi kusimama peke yake bila kijalizo chake. Brinton (2000) anabainisha sifa hii kwa kueleza kwamba neno kuu la KH ni kihusishi, lakini ni tofauti na kategoria nyingine za virai kwani kihusishi hakiwezi kusimama peke yake, lazima kiambatane na KN ambacho kimapokeo kinajulikana kama yambwa ya kihusishi.

**4.2.5. KH Kuundwa na Vipashio vya Kileksika na/au vya Kisintaksia**

Makala haya yamebaini kwamba, kimuundo, KH kina sifa ya kuundwa na vipashio vya kategoria za kileksika, kirai na kishazi. Kwa upande wa neno kuu, vipashio lazima viwe vya kategoria ya kileksika na viwe neno moja. O'Grady (1996) anaeleza kwamba kategoria ni kiwango cha neno mojamoja la kileksika ambalo linaweza kuwa nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi au kihusishi. Kwa upande wa kijalizo, vipashio vinaweza kuwa vya kileksika au kirai kama Data Na.8 na 9 zinavyoonesha.

8. (a) ya nyumba
   (b) katika nyumba
   **Chanzo:** Amidu (2004: 50)

9. (a) kwa fedha taslimu
   (b) kwa shemeji yake
   (c) Mtu aliye kando haangukiwi na mti wowote.
   **Chanzo**: Kapinga (1983:186-187)

Tungo zilizopigiwa mistari katika Data Na. 8 (a)-(b) ni virai vihusishi vilivyoundwa kwa maneno ya kategoria ya kileksika, yaani vihusishi [ya, katika, kwa] kwa upande wa neno kuu na kategoria ya nomino [nyumba, samaki] kwa upande wa vijalizo. Data Na. 9 (a) na (b) inaonesha kwamba virai vihusishi vina maneno makuu ambayo ni vipashio vya kategoria ya kileksika na virai nomino [fedha taslimu, shemeji yake] ambavyo ni kategoria za virai. Aidha, katika Data Na. 9(c) kuna sentensi yenye kirai kihusishi [na mti wowote] kilichoundwa na neno kuu [na] ambalo ni la kategoria ya kileksika, na vijalizo vyake ambavyo ni virai nomino vilivyoundwa na nomino na kivumishi [mti wowote].

**4.3 Sababu za Kiisimu za Wataalamu Kutofautiana Kiuchanganuzi**

Kutokana na data, makala haya yamebaini sababu mbili kuu zinazowafanya wataalamu wa sarufi ya Kiswahili watofautiane kiuchanganuzi kuhusu KH cha

Kiswahili. Sababu hizo ni athari za tafsiri kutoka katika lugha za kigeni pamoja na kutozingatiwa kwa Kanuni za Sarufi Miundo Virai (kuanzia sasa KSMV).

**4.3.1 Athari ya Tafsiri ya Vihusishi kutoka Lugha za Kigeni**

Makala haya yamebaini kwamba sababu mojawapo ya kiisimu inayowafanya wataalamu wa sarufi watofautiane kiuchanganuzi kuhusu KH cha Kiswahili ni athari ya tafsiri ya vihusishi kama maneno makuu kutoka katika lugha za kigeni kama vile Kiingereza. Data Na. 10 inadhihirisha wazi athari hiyo.

10. (a) *between* - kati ya
    (b) *behind* - nyuma ya
    (c) *on* - juu ya
    **Chanzo:** Habwe na Karanja (2004: 190)

Data Na. 10 inaonesha kuwa vihusishi vya Kiingereza vimetafsiriwa katika Kiswahili na kupatikana vihusishi vya Kiswahili vyenye maneno zaidi ya moja kama vile: *kati ya*, *nyuma ya* na *juu ya.*

Katika kuchanganua virai vihusishi, wataalamu wa sarufi ya Kiswahili wanatofautiana. Kuna wale wanaoamini kwamba maneno hayo mawili yaliyotafsiriwa ni vihusishi ilhali wengine wakiamini kwamba kihusishi katika maneno hayo ni *ya* peke yake. Kiango (2008) anaeleza kwamba watumiaji wa lugha ya Kiswahili wanaofanya kazi za tafsiri na utangazaji wamebuni maneno ya kutekeleza kazi zao na matokeo yake ni kwamba Kiswahili kimejazwa maneno mengi ambayo yamekifanya kionekane kigumu na kigeni hasa kwa watu ambao hawakujiandaa kwa mabadiliko haya. Maelezo hayo ya Kiango yanathibitisha wazi kwamba mtazamo wa wataalamu wanaoona kuwa kihusishi cha Kiswahili ni kifungu cha maneno badala ya neno moja umetokana na athari ya tafsiri kutoka katika lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, kihusishi ambacho ni neno moja katika lugha ya Kiingereza hakiwezi kutafsiriwa kwa neno moja katika lugha ya Kiswahili. Aidha, Steere (1884) na Le Breton (1948) wanaelekea kuwa na mtazamo kama huu wanapoeleza kwamba lugha ya Kiswahili ina vihusishi halisi vichache ambavyo si zaidi ya vinne, yaani *na*, *ya*, *kwa* na *katika.* Steere (1884) anaendelea kueleza kwamba vihusishi vya Kiswahili kama vile "tangu" au "tokea" vimetafsiriwa kutoka katika kihusishi cha Kiingereza, yaani 'from'. Hivyo, wataalamu wa sarufi ya Kiswahili wanaweza kutofautiana kiuchanganuzi kuhusu KH kutokana na athari ya tafsiri ya vihusishi kutoka katika lugha za kigeni.

**4.3.2 Kutozingatiwa kwa Kanuni za Sarufi za Miundo Virai**

Kutokana na uchambuzi wa data, makala haya yamebaini kwamba sababu nyingine inayowafanya wataalamu wa sarufi ya Kiswahili watofautiane kiuchanganuzi kuhusu KH ni kutozingatiwa kwa KSMV. Wataalamu wanaochanganua KH cha Kiswahili kwa kuzingatia kihusishi cha neno moja la kileksika kama neno kuu na KN kama kijalizo chake wanazingatia kanuni ya neno kuu pamoja na kategoria ilhali wale wanaochanganua KH cha Kiswahili chenye kihusishi cha maneno

mawili, yaani neno huru zaidi ya moja na KN hawajazingatia KSMV hususani kanuni ya neno kuu na kanuni ya kategoria kama inavyoonekana katika Data Na.11.

11. la, ya, cha, vya, wa, za, kwa, pa, mwa
 **Chanzo:** Wesana-Chomi (2017: 103)

Data Na.11 inaonesha kwamba vihusishi vimeundwa na neno lenye kategoria moja. Muundo huo wa vihusishi umefuata KSMV ambazo zinaelekeza kwamba neno kuu lazima liundwe na neno moja ambalo ni la kategoria moja tu.

Kwa upande mwingine, wataalamu wanaochanganua KH cha Kiswahili chenye kihusishi cha maneno mawili na KN hawajazingatia kanuni ya neno kuu na kategoria. Kanuni hizi zinahitaji neno kuu kuwa neno moja tu lakini uchanganuzi wa wataalamu hao unaonesha maneno mawili yenye kategoria zaidi ya moja. Data Na. 12 inaonesha vihusishi vyenye maneno zaidi ya moja ambavyo muundo wake umekiuka kanuni ya neno kuu na kategoria.

12. (a) <u>mbele ya</u> ikulu
 (b) <u>nyuma ya</u> darasa
 (c) <u>wakati wa</u> pasaka
 **Chanzo:** Habwe na Karanja (2004: 190)

Data Na.12 inaonesha virai vihusishi vilivyoundwa na vihusishi ambavyo vimepigiwa mistari kama maneno makuu. Vihusishi hivyo ni maneno mawili. Kwa kawaida, neno kuu linapaswa kuwa neno moja lenye kategoria moja na sio maneno mawili yenye kategoria zaidi ya moja. Muundo huo wa virai vihusishi umekiuka kanuni ya neno kuu na kategoria. Hivyo, uchanganuzi huo wa wataalamu kuhusu KH cha Kiswahili unatofautiana kutokana na kutozingatiwa kwa KSMV na matokeo yake ni kukosekana kwa urari wa kiuchanganuzi kuhusu KH cha Kiswahili.

## 5.0 Hitimisho

Kwa ujumla, makala haya yamebainisha muundo wa KH cha Kiswahili na kueleza sifa za kimuundo za kirai kihusishi. Pia, yamefafanua sababu za kiisimu zinazowafanya wataalamu wa sarufi ya Kiswahili watofautiane kiuchanganuzi kuhusu KH. Kutokana na uchanganuzi wa data, makala haya yanaunga mkono mtazamo kwamba KH kina muundo wa kihusishi (H) kama neno kuu na kirai nomino (KN) au kishazi tegemezi (Kg) kama kijalizo cha kihusishi. Mtazamo huu umeungwa mkono kwa sababu umekidhi sifa za kimuundo za KH cha Kiswahili. Sifa hizo ni: neno kuu la kirai kuwa kihusishi; neno kuu kutawala vijalizo vyake; neno kuu kutangulia kijalizo chake; neno kuu kutosimama peke yake, na KH kuundwa na vipashio vya kategoria ya kileksika kwa upande wa neno kuu na/au kirai, kishazi huru au kishazi tegemezi kwa upande wa kijalizo. Aidha, makala haya yamebaini kuwa sababu zinazowafanya wataalamu wa sarufi watofautiane kiuchanganuzi kuhusu KH cha Kiswahili ilhali wanatumia mkabala mmoja wa

SMV ni athari za tafsiri ya vihusishi kutoka lugha za kigeni na kutozingatiwa kwa KSMV. Hivyo, uchanganuzi wa KH cha Kiswahili unapaswa kuzingatia KSMV ili kuwe na urari wa kiuchanganuzi.

**Marejeleo**

Amidu, A.A. (2004) “Kiswahili Language Description and Translational Grammars”. *Taiwan Journal of Linguistics*, Juz. 2: 45-64.

Baker, C.L. (1995) *English Syntax, Toleo la Pili*. London: MIT Press.

Brinton, L.J. (2000) *The Structure of Modern English: A Linguistic Introduction*. Amsterdam/Philadelphia: John Benjamins Publishing Company.

Chomsky, N. (1957) *Syntactic Structures.* New York: Mouton de Gruyter.

Downing, A. (2015) *English Grammar: A University Course Toleo la Tatu*. London/New York: Routledge.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Hassan, F. (2021) “Mikabala ya Uchanganuzi wa Viambajengo vya Sentensi na Istilahi Zinazotumika: Mifano kutoka Lugha ya Kiswahili”. *Mulika*, Juz. 40: 1-22.

Kapinga, M.C. (1983) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: TUKI.

Khamis, A.M (2009) *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Sarufi I*. Dar es Salaam: TUKI.

Kiango, J.G. (2008) (Mh.) *Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Kihore, Y.M. (2009) *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Sarufi II*. Dar es Salaam: TUKI.

Kimani, N., Mwihaki, A. na Buliba, A. (2006) *Sarufi ya Kiswahili Uchanganuzi na Matumizi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Le Breton, F.H. (1948) *Up-Country Swahili Exercises for the Soldier, Settler, Miner, Merchant and their Wives and for all Dealing with Up-Country Natives without Interpreters*. London: RW Simpson and Co. Ltd.

Matei, A.K. (2008) *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Ramco Printing Works Ltd.

Matinde, S.R. (2012) *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Miller, J. (2002) *An Introduction to English Syntax*. Edinburg: Edinburgh University Press.

Mychina, E.N. (1981) *The Swahili Language: A Descriptive Grammar*. London, Boston and Henley: Routledge and Kegan Paul Ltd.

O’Grady, W. na Archibald, J. (Wah.) (2016) *Contemporary Linguistics Analysis: An Introduction. Toleo la Nane*. Toronto: Pearson Canada Inc.

Obuchi, M.S. na Mukhwana, A. (2015) *Muundo wa Kiswahili Ngazi na Vipengele.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

OUT (2018) OFP *008 Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Rubanza, Y.I. (2003) *Sarufi Mtazamo wa Kimuundo*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Tallerman, M. (2015) *Understanding Syntax, Toleo la Nne*. New York: Routledge.

Trask, R.L. na Stockwell, P. (2007) *Language and Linguistics: Key Concepts*. New York: Routledge.
TUKI (2019) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
Wesana-Chomi, E.W. (2017) *Kitangulizi cha Muundo Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.